

**TANGAZO LA MAENEKO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA  
KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM**

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEKO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Bweni Na. III	Kampasi ya Mlimani	Saluni ya Kike
2.	Bweni Namba IV	Kampasi ya Mlimani	Steshenari na kuchapisha nyaraka, kadi za mwaliko n.k.
3.	Chumba Namba 5 Mabibo Shopping Complex	Hosteli za Mabibo	Saluni ya Kiume
4.	Chumba Namba 6 Mabibo Shopping Complex	Hosteli za Mabibo	Duka la vinywaji baridi na mahitaji madogo madogo
5.	Chumba Namba 10 Mabibo Shopping Complex	Hosteli za Mabibo	Saluni ya Kike
6.	Chumba Namba 4	Kampasi ya Kijitonyama	Huduma za kifedha (Mpesa, Tigo pesa, Airtel Money, wakala wa benki)

Kwa tangazo hili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Mendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 303 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (10,000/=) kupitia ‘Namba ya Kumbukumbu’ ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe 7 Machi 2022 itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi tutakutana katika Kampasi ya Kijitonyama, saa 6:00 mchana tutakutana katika Hosteli za Mabibo na kuanzia saa 8:00 mchana tutakutana katika Kampasi ya Mlimani ya Mwalimu J.K. Nyerere.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

***Imetolewa na***  
***NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO, UTAWALA***  
***23.2.2022***